

**TANZANIA BİRLEŞİK
CUMHURİYETİ
BÜYÜKELÇİLİĞİ
TÜRKİYE**



**EMBASSY OF THE
UNITED REPUBLIC
OF TANZANIA
TÜRKİYE**

In Reply please quote:

Kumb. Na. KAJ.590/649/01/114

08 January, 2024

Katibu Mkuu,
Wizara ya Mambo ya Nje na
Ushirikiano wa Afrika Mashariki,
Mji wa Serikali, Mtumba,
S.L.P 2933,
40466 DODOMA.

**Yah: FURSA ZA UDHAMINI WA MASOMO KWA MWAKA 2024/2025 NCHINI
UTURUKI**

Tafadhali rejea somo tajwa hapo juu.

2. Ubalozi unapenda kukujulisha kwamba umepokea orodha ya Taasisi za Serikali na zisizo za Kiserikali zinazotoa Udhamini wa masomo nchini Uturuki. Udhamini huo wa masomo ni kwa ajili ya wanafunzi wa mataifa ya nje kwa mwaka 2024/2025 katika ngazi ya Shahada, Uzamili na Uzamivu. Maombi ya Udhamini yanafunguliwa tarehe 10 Januari, 2024 na kufungwa tarehe 20 Februari, 2024.
3. Taasisi ambazo zinatoa udhamini wa masomo hayo ni kama ifuatavyo;
 - i. Türkiye Bursları <https://www.turkiyeburslari.gov.tr>
 - ii. Diyanet Burslari-Türkiye Diyanet Vakfı <https://diyanetburslari.tdv.org>
 - iii. Islamic Development Bank <https://www.isdb.org/scholarships>
4. Ubalozi unashauri kwamba ni vema taarifa hizi ziwafikie walengwa ili waweze kunufaika na fursa hii ya udhamini wa masomo, ambapo mwaka 2023/2024 Tanzania ilipata fursa za udhamini wa masomo kwa wanafunzi 51 kusoma katika vyuo mbali mbali nchini Uturuki.
5. Tunashukuru kwa Ushirikiano wako.


Iddi Seif Bakari
BALOZI